SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No.15 June 2024

# Dhima ya Ushikamani wa Mandhari na Jukwaa la Kisasa katika Maigizo Teule ya Kiswahili ya Studioni

Dkt. Nawaje Ali Mganga
Mhadhiri na Mudiri wa Idara ya Lugha, Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait
*nawajea@gmail.com*

&

Wasila Makame Ali
Mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro
*wasilas82@gmail.com*

*Received: 1 May 2024, Accepted: 1 May 2024, Published June 2024*
*© SUMAIT University Journal 2024*

**Abstract**

*Due to the development of science and technology influenced by globalization in African societies, including Tanzania, studio acting has emerged. This has caused difficulty in distinguishing the border of the stage and the scene of the dramas. This is because the part that was used as a stage in the past, that is the part that rose in the hall in front of the audience as they say (Mugubi and Kebaya, 2012), is currently no longer used; even when it is used, it is not a theater for acting but a theater to show the drama recorded in technological tools such as television, computer and video recorder (Wanjala and Kavoi, 2011). Thus, the analysis of the elements of the scene and the modern stage in Kiswahili dramas has been controversial, because the place where there should be a stage is where the scene appears. Therefore, the article has identified the role of the cohesion of the scene and the modern stage in the Kiswahili dramas of the studio in order to introduce the importance of that cohesion. If the research of this article had not been done, the audience of Kiswahili dramas as well as the critics would have continued not to see the roles of the cohesion of those elements in studio dramas.*

***Ikisiri***

*Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyochagizwa na utandawazi, katika jamii za Afrika, ikiwamo Tanzania, kumeibuka uigizaji wa studioni. Jambo hilo limesababisha ugumu wa kupambanua mpaka wa jukwaa na mandhari ya igizo. Hii ni kwa sababu sehemu iliyokuwa ikitumika kama jukwaa hapo zamani, yaani sehemu maalumu iliyoinuka ukumbini mbele ya hadhira kama wasemavyo (Mugubi na Kebaya, 2012), kwa sasa haitumiki tena; hata inapotumika haiwi sehemu ya kuigizia bali ni ukumbi wa kuoneshea igizo lililorekodiwa katika zana za kiteknolojia kama vile runinga, tarakilishi na kinuruweo (Wanjala na Kavoi, 2011). Hivyo, uchambuzi wa vipengele vya mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya Kiswahili umekuwa na utata, kwani pahala panapopaswa kuwa jukwaa ndipo hapohapo huibua mandhari. Kwa hivyo, makala imebainisha dhima ya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya Kiswahili ya*

*studioni ili kuutambulisha umuhimu wa ushikamani huo. Kama utafiti wa makala hii usingefanyika, hadhira ya maigizo ya Kiswahili pamoja na wahakiki wangeendelea kutoona dhima za ushikamani wa vipengele hivyo vya kifani katika maigizo ya studioni.*

**Keywords**: Ushikamani, Mandhari, Jukwaa, Maigizo.

## Utangulizi

Mandhari ni miongoni mwa vipengele muhimu vya fani katika kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa Donna (1992), mandhari ni uti wa mgongo wa kazi yoyote ya fasihi kwa vile humwezesha msanii kujenga hisia kwa hadhira kwa kuyahusisha matukio na mazingira lengwa. Anaendelea kufafanua kuwa mandhari hushirikisha vipengele kadhaa katika kuisana kazi ya fasihi ili kuibua mwonekano na makusudio ya mtunzi wa kazi ya fasihi. Mandhari huundwa na mahali na wakati ambao tukio la kifasihi husanwa na kutendeka (Wamitila, 2002). Kwa maana hiyo, mandhari hufanikisha ujenzi wa kazi ya fasihi kupitia sehemu, wakati, tukio na watendaji. Vipengele hivi vinavyojenga mandhari vina ukaribu mkubwa na vipengele vinavyounda jukwaa katika maigizo ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu jukwaa hilo huhusisha mahali ambapo kazi ya fasihi inatendeka.

Jukwaa ni dhana pana ambayo huweza kuelezwa kwa namna tofauti. Kwa mfano, Wamitila (2003) anaeleza kuwa, jukwaa linaweza kuwa ndani au nje ya jengo maalumu, ambapo huwa na mwinuko kiasi cha hadhira kupata fursa ya kuona kinachoigizwa. Hii ni kwa sababu kumbi za maigizo huwa na halaiki ya watu. Maelezo haya yanasawiri ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya kigeni kabla ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hivi leo, katika kumbi za maigizo jukwaa linaweza kuwa chini na vikalio vya hadhira vikawa juu, ilimradi uwasilishaji wake unawafikia hadhira.

Kwa asili, jukwaa la kijadi la Kiafrika lilitegemea utendaji wa sanaa za maonesho ya kidini, tanzu za fasihi simulizi na matukio mengine ya kijamii. Utendaji wake ulikuwa wa moja kwa moja pamoja, uliosheheni ufaraguzi na kuhusisha shughuli za muziki, wimbo, densi na tamasha (Kahuro, 2018). Matambiko ya kijadi katika makabila yalijumuisha mavazi, mapambo, muziki, ngoma, hotuba rasmi, nyimbo, pamoja na vifaa maalumu kama vile fimbo, mikuki, mafuvu, njuga na kadhalika.

Kwa upande wa Afrika ya Mashariki, mathalani nchini Kenya, jukwaa la sanaa za maonesho lilianza zamani kabla ya ujio wa wakoloni. Jukwaa hilo lilijulikana kama jukwaa asilia la Afrika, ambapo jamii ziliigiza shughuli au matendo yao ya kila siku wakiwa hadharani (Mugubi na Kebaya, 2012). Maelezo hayo yanamaanisha kwamba jukwaa la asili halikuwa na jengo maalumu wala mwinuko wowote, ila ni sehemu tu ya kuigizia maisha halisi. Baada ya ujio wa wakoloni, wenyeji walivunjika moyo katika matumizi ya jukwaa la asili, kwani walilazimishwa waigize sanaa za kigeni katika kumbi maalumu au majengo ya kanisa (Mugubi na Kebaya, wameshatajwa). Kuanzia hapo, ndipo jukwaa la kijadi likabadilika na kuwa jukwaa la kisasa lililoibua maigizo mapya.

Maigizo ni sanaa inayotumia waigizaji kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kufikisha ujumbe. Kwa maana, maigizo ni sanaa yenye mpangilio wa maneno yaliyo katika matendo ya wahusika, ambayo hutendwa jukwaani mbele ya hadhira (Mulokozi, 2017). Maigizo ya kijadi ya Kiswahili barani Afrika yaliambatishwa na ngoma, utambaji wa hadithi na sherehe za

kiutamaduni, huku waigizaji wakiwa wamevaa maleba maalumu na utendaji wake mbele ya hadhira ulihusisha na tanzu nyengine za fasihi simulizi (Samwel, 2015). Maelezo haya yanaonesha historia fupi ya maigizo asilia ya Kiafrika, ambapo uwasilishaji wake ulikuwa wa ana kwa ana. Hivyo, hata jukwaa lake lilikuwa bayana; yaani, lilijipambanua kimwonekano na kimatumizi, kama wasemavyo Njogu na Chimerah (1999) kuwa kuigiza ndiyo msingi wa maigizo, jukwaa ni muhimu sana katika kufanikisha utanzu huu. Hivyo, mtu hawezi kuzungumzia maigizo bila ya wazo la jukwaa kulitilia maanani.

Mganga (2021) ameainisha maigizo ya Kiswahili katika nui tatu ambazo ni: maigizo ya watoto, maigizo ya jukwaani na maigizo ya studioni. Uainishaji huu umetoa fursa ya kuyatambua maigizo ya zamani na ya kisasa. Maigizo ya zamani ni yale yanayotumia jukwaa maalumu lenye sura ya mwinuko kama alivyobainisha Wamitila (keshatajwa). Kwa upande wake, maigizo ya kisasa ni yale aliyoyaweka Mganga (keshatajwa) katika nui ya maigizo ya studioni. Jukwaa lake ni tofauti na jukwaa la maigizo ya zamani, kwani jukwaa la maigizo ya zamani huwa sehemu maalumu ambayo huteuliwa na waigizaji ambapo kila tukio hutendekea hapo. Pia, hadhira huwa ana kwa ana na waigizaji. Jukwaa la studioni huwa sehemu yoyote ambayo mtunzi huichagua kulingana na tukio la uigizaji linalotendeka. Pia, mtunzi hurekodi maigizo na kutazamwa na hadhira kupitia runinga au vifaa vingine vya kielektroni pamoja na mitandao ya kijamii kama vile *youtube*.

Kwa kuwa kuna maigizo ya studioni, jukwaa limepata sura nyingine inayoweza kuleta ugumu katika upambanuzi wake, ikihusishwa na mandhari ya kazi ya fasihi. Hii ni kwa sababu maigizo ya kisasa hurekodiwa studioni kupitia mahali kama vile sokoni, darasani na chumbani. Swali linaloweza kuibuka ni je, sehemu hizo zitambulike kama jukwaa au mandhari? Hivyo, mpaka uliopo baina ya mahali panapoonesha jukwaa au mandhari katika maigizo ya Kiswahili unakuwa mgumu kiuchambuzi.

Ifahamike kuwa kwa sasa maigizo ya Kiswahili yamepata sura mpya katika uwasilishwaji wake kutokana na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia. Hapo awali, maigizo ya Kiswahili yalikuwa yakiigizwa mbele ya hadhira, tena jukwaani. Hadhira hiyo huwa mbele ya waigizaji. Maigizo ya kisasa huwasilishwa kupitia runinga, redio na mitandao ya kijamii au hata kuandikwa vitabuni. Hali hiyo imesababisha ugumu wa kubainisha mahali pa jukwaa na mandhari. Kwa maana hiyo, dhima ya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya Kiswahili hauna budi kuwekwa bayana. Hii ndiyo sababu iliyomfanya mtafiti kuchunguza dhima ya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya Kiswahili.

## Kiunzi cha nadharia

Makala hii imechunguza dhima ya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo teule ya Kiswahili ya studioni. Maigizo hayo ni **Bado Natafuta** na **Safari ya Gwalu**. Utafiti wa makala hii, uliongozwa na nadharia ya Uamilifu. Nadharia hii hutumika kurejelea mawazo kulingana na muktadha wa matumizi husika (Kobia, ht). Nadharia ya Uamilifu iliasisiwa na Bauman anayesisitiza kwamba mhakiki hana budi kuchunguza matini kupitia muktadha wake halisi (Bauman, 1989 na Wanjala, 2011). Tuliichagua nadharia hii kwa kuwa inasisitiza kuwa utendaji ni uti wa mgongo wa utanzu wa maigizo kupitia vipengele vya mandhari na jukwaa. Uchambuzi ulitumia mhimili wa Dhima ya fasihi: Dhima ya uamilifu katika kazi ya fasihi hufasiriwa kulingana na mila na desturi za jamii husika. Ulimsaidia mtafiti kubainisha dhima za ushikamani wa mandhari

na jukwaa la kisasa katika maigizo ya Kiswahili kwa kuwa dhima hutegemea utamaduni wa jamii husika.

## Methodolojia ya utafiti

Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili na mijadala ya vikundi lengwa. Mkabala wa kitaamuli ulitumika katika uchambuzi wa data. Utafiti wa makala hii umefanyika mkondoni na uwandani. Kupitia mkondoni, mtafiti aliangalia maigizo teule katika mtandao wa kijamii wa *Youtube*. Maigizo hayo yaliwekwa katika matukio mafupifupi kiasi cha kumfanya mtafiti asichoke kutazama ili kuweza kupata mifano ya hoja za utafiti. Kwa upande wa uwandani, utafiti wa makala hii ulifanyika katika Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar. Sababu za kuchagua eneo hilo ni: Mosi, kunapatikana kwa Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), ambako kozi ya maigizo ya Kiswahili hufundishwa. Pili, mtafiti alichagua eneo hilo kutokana na urahisi waupatikanaji wa sampuli ya utafiti wa makala hii kama vile kuwapo kwa Baraza la Sanaa, Sensa za Filamu na Utamaduni (BASSFU). Pia, Skuli ya Sekondari ya Kiponda ambayo ni skuli pekee inayofundisha tahasusi ya lugha na sanaa kwa Zanzibar. Vilevile, eneo hilo hupatikana wasanii wengi kiasi wenye kupenda kuigiza, kutunga na kutazama maigizo ya Kiswahili.

## Muhtasari wa maigizo teule

Bado Natafuta ni igizo lililoandaliwa na kampuni ya Jerusalem, kwa ufadhili wa kampuni ya Pepsi, chini ya mwongozaji wa filamu anayejulikana kwa jila la Jacob Steven (JB). Igizo hili lilianza kurushwa mwaka (2014). Mtunzi wa igizo hili ni Daniel Manage. Maudhui ya igizo hili ni kuwapa moyo watu wa tabaka la chini kuhusu harakati za kupambana na maisha, ikiwa ni pamoja na kuwa na familia bora, maisha mazuri na kuheshimiwa. Igizo hili, limegawika sehemu mbili kuu. Kila sehemu imegawika mara mbili; sehemu ya 1A na 1B na sehemu ya 2A na 2B. Sehemu zote hizo, zimeundwa na matukio yenye kuchukua muda wa dakika 30 kwa kutazamwa. Igizo hili lilishawahi kupata tuzo ya filamu bora mwaka (2016) kutoka kituo cha East African Television.

Kwa upande mwengine, Safari ya Gwalu ni igizo lililotungwa na Daniel Manage mwaka (2015). Mwongozaji wa igizo hili ndiye huyohuyo mtunzi mwenyewe chini ya kampuni ya D. Magic Entertainment. Maudhui ya jumla ni kuwapa matumaini watu wa tabaka la chini kuwa wanaweza, pale watakapoamua kujikita katika jambo, kama vile masuala ya kielimu, kiuchumi na kijamii. Igizo hilo lilipata tuzo ya filamu bora mara mbili: Mwaka (2016) kutoka *Zanzibar International Film Festival Awards* (ZIFF) na mwaka (2018) kutoka *Sinema Zetu International Film Festival* (Issa, 2023). Mambo hayo yote yalionekana kupitia ushikamani mzuri wa mandhari na jukwaa la kisasa katika igizo hilo.

## Matokeo ya utafiti

Sehemu hii imewasilisha dhima ya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo teule ya Kiswahili ya studioni. Dhima hizo ni pamoja na kujenga uhalisi, kuleta mvuto kwa hadhira, kujenga taharuki pamoja na kudhihirisha maendeleo ya maigizo ya Kiswahili. Uchambuzi ufuatao unathibitisha:

**Kujenga Uhalisi**

Katika zama hizi za utandawazi, maigizo huwasilishwa kwa njia ya runinga na mitandao ya kijamii (Qassim, 2022). Hii inamaanisha kwamba kushikamanishwa kwa vipengele vya mandhari na jukwaa la kisasa katika uwasilishaji wa maigizo kunaendana na hali halisi ya maigizo hayo. Hii ni kwa sababu hivi sasa maigizo hayawasilishwi kwa njia za asili mbele ya hadhira, bali huwasilishwa kwa zana za sayansi na teknolojia. Hivyo, hakuna nafasi ya kutenganisha vipengele vya mandhari na jukwaa la kisasa. Suala hili linaafikiana na nadharia teule ya makala hii kupitia mhimili unaofafanua kuna dhima ya fasihi. Hapa dhima ya ushikamani wa mandhari na jukwaa la Kisasa katika maigizo teule ya Kiswahili ya studioni imefasiriwa kulingana na mila na desturi za jamii husika. Mathalani, maigizo teule yamewasilishwa kwa njia ya video. Zifuatazo ni picha zinazoonesha sehemu ya video hizo:




**Picha na. 1 & 2, zinazoonesha sehemu za video katika maigizo teule.**

Picha hizo ni nakala halisi ya picha mwendo (video) ambayo imenaswa katika hali ya picha tuli ili kuweza kuwasilishwa katika makala hii. Dakika zilizomo katika picha hizo ni ithibati ya wakati wa sehemu ilipofikia video ya igizo husika. Hivyo, ushikamani wa mandhari na jukwaa la Kisasa katika maigizo teule ya Kiswahili ya studioni umeweza kuisawiri hali halisi ya maigizo ya kisasa katika jamii. Vilevile, mtoa taarifa 3 anaeleza dhima ya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo teule ya Kiswahili ya studioni kwa kusema:

> Kushikamana kwa mandhari na jukwaa la Kisasa katika maigizo teule ya Kiswahili ya studioni ndio uhalisi ulivyo, kwa sasa maigizo hayawasilishwi tena katika kumbi za maonesho, kwani mambo yamerahisishwa na zana za sayansi na teknolojia. Hii inamaanisha kuwa vituo vya televisheni na mitandao ya kijamii ndio njia zinazotumika kuyawasilisha maigizo hayo. Kwa mfano, kuna chaneli maalumu za maigizo katika visimbuzi vyetu hapa nchini. (Mjadala wa Kikundi 2, Mtoa taarifa 3, 30/3/2023)

Maelezo hayo yanamaanisha kuwa ushikamani wa mandhari na jukwaa la Kisasa katika maigizo teule ya Kiswahili ya studioni yana dhima ya kuisawiri hali halisi ya maigizo ya Kiswahili; maigizo yameathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia au utandawazi kwa vile huwasilishwa kupitia zana za kisayansi ambazo hazitoi nafasi kwa vipengele vya mandhari na jukwaa la kisasa kutenganishwa.

### Kuleta Mvuto kwa Hadhira

Mvuto wa sanaa hutokana na jinsi wahusika wanavyoigiza, matukio yalivyopangwa, uteuzi mzuri wa mandhari kulingana na tukio la utendaji, na hata lugha itumiwayo na waigizaji kwa lengo la kufikisha ujumbe. Kadhalika, waigizaji hupaswa kulitawala vyema jukwaa la maigizo pamoja na mandhari iliyoandaliwa ili kuwafanya watazamaji waweze kuvutiwa na tukio linaloigizwa. Hali hiyo husababisha ujumbe kufika kwa haraka kwa walengwa husika. Hivyo, ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya teule ya Kiswahili ya studioni ni nyenzo kwa waigizaji ili kuibua dhima ya mvuto kwa watazamaji wa igizo husika. Kama inavyofafanua nadharia teule ya utafiti unaoripotiwa katika makala hii kupitia mhimili unaoelezea dhima ya fasihi, kuwa utamaduni una nafasi katika jamii. Hapa dhima ya fasihi hufasiriwa kulingana na mila na desturi za jamii. Hivyo, ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya teule ya Kiswahili ya studioni huibua dhima yake kulingana na utamaduni wa jamii lengwa. Mfano ufuatao unatoka katika igizo la *Safari ya Gwalu*:

> (Tupac aliingia darasani akiwa amejifunga kilemba usawa na paji lake la uso, huku akitembea kama kwamba hakuna anayemwogopa. Ndipo mwalimu wa darasa aliyekuwa kwenye kipindi alimsimamisha na kumuuliza)
>
> **Mwalimu:** Wee! Tupac wiki nzima sijakuona darasani ulikuwa wapi?
>
> **Tupac:** Nilikuwa natengeneza pesa mwalimu.
>
> **Mwalimu:** Bila ya elimu hamna pesa, Tupac njoo shule kwanza usome ili upate hela. Na hichi kitambaa vipi?
>
> **Tupac:** Kitambaa changu cha kufutia makamasi mwalimu.
>
> **Mwalimu:** Nisikuone nacho tena darasani.
>
> **(Igizo la Safari ya Gwalu, sehemu 2, dk. 15: 10)**

Nukuu hiyo imeshikamanisha vipengele vya mandhari na jukwaa la kisasa katika igizo hilo. Yaani, mandhari na jukwaa la kisasa yamebebanishwa kwa pamoja, hatimaye yakaibua dhima ya kuleta mvuto kwa watazamaji wa maigizo husika. Mtunzi amefanikiwa kumchora mhusika, kijana wa mtaani asiyekuwa na maadili, huku akihudhuria shule kwa kudonoadonoa. Kitendo cha Tupac kujiwa kama mtoto asiyeambilika wala kujali heshima kwa mwalimu wake, na mwalimu wake akatumia nafasi yake ya ualimu kumkataza, kinaleta mvuto kwa mtazamaji kwa vile hilo ni miongoni mwa mambo yanayoitesa jamii kutokana na mmong'oonyoko wa maadili. Nadharia ya Uamilifu kupitia mhimili unaofafanua dhima ya fasihi. Katika jamii ya Watanzania, kijana wa kiume haruhusiwi kujifunga kitambaa kichwani wala kutoroka skuli, kwani huashiria kuwa ni utovu wa maadili.

Katika igizo la ***Bado Natafuta*** msanii anadokeza kwa kusema:

> **James:** Moyo wangu umekubali kusamehe kwa yote yaliyopita. Kwa nini moyo wako usisamehe?... Nilikwambia siku moja baba yako anaweza kurudi. Mimi ndo baba yako.
>
> **Karo:** Sasa we uliniongopea. Mimi siku zote nilijuwa wewe ndio Anko rafiki.
>
> **James:** Hivi ningekwambia kuwa mimi baba yako bila ya kukwambia mama yako ungeniamini. Siku zote nakwambia kila wanaloongea wazazi wako ni la kweli lakini muda mwingine lazima utumie nini.
>
> **Karo:** Akili

**James:** Ndio akili inayoweza kupambanua majambo. Lakini moyo huweza kugusa hisia. Kwa muda wote huo hisia zangu ziliweza kukupenda, na wewe ulinipenda na ndio maana tukawa tunaelewana. Endelea kuwasikiliza wazazi wako. Leo nimekuletea zawadi.
**Karo:** Utakuja nyumbani?
**James:** Nilikwambia kama mama yako ataniruhusu basi nitakuja.
**(Bado Natafuta, sehemu 2B, dk. 24: 30 – dk. 25: 50)**

Maelezo hayo, yameambatisha ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa na yakaibua hisia nzito alizokuwa nazo James juu ya familia yake. Familia ambayo ilijitenga naye na kuishi na mwanamme mwingine bila ya kujali kuwa yeye ndiye baba wa mtoto na pia ni mume wa Patricia. Suala hilo na hisia nzito, pia zitampata mtazamaji wa igizo hilo kwa kuwa mambo ya upendo wa familia ndio suala muhimu kwa binadamu yeyote. Kwa maana ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa uliopo umeweza kuvuta hisia kwa watazamaji wa igizo kutaka kujua hatima ya James na Patricia itakuwaje. Mtoa taarifa 10 anaeleza:

> Uziaaji mzuri wa vijenzi vya mandhari na jukwaa la maigizo husababisha igizo kuwa na mvuto wa mnato kwa watazamaji wake. Hii ni kutokana na kuwa jamii hupendezewa kuangalia maigizo yenye mshikamano mzuri wa mandhari halisi na jukwaa la kuigizia. (Mjadala wa Kikundi 2; Mtoa taarifa 10, 30/3/2023)

Maelezo hayo yanamaanisha kuwa ushikamani wa vijenzi vya mandhari na jukwaa la kisasa katika uigizaji husababisha maigizo hayo kuwa na mvuto kwa hadhira lengwa. Yaani, mandhari na jukwaa la kisasa yakisadifiana basi dhima ya mandhari na jukwa la kisasa inaoana na utamaduni wa hadhira na kusababisha igizo husika kuleta mvuto kwa hadhira na kusababisha kupokelewa vyema na jamii, kama nadharia ya Uamilifu katika mhimili teule inavyofafanua kuwa utamaduni una dhima katika fasihi, na kwa muktadha huu maigizo ya Kiswahili.

**Kujenga Taharuki**

Kwa mujibu wa Madumulla (2009), taharuki ni hali ya msanii kupanga kazi yake kiasi kwamba tukio moja linasababisha jingine, na kusababisha kujenga hamu ya mtazamaji ya kutaka kuendelea kujua kwa nini. Hii ina maana ya kwamba, mtazamaji hupata shauku ya kujua mwendelezo wa kinachofuata hali hiyo ndio huitwa taharuki. Sambamba na hayo, taharuki katika sanaa ya maigizo hutumia mbinu anuwai ili kuvuta hisia na usikivu wa watazamaji. Hali hiyo huifanya hadhira kujiuliza maswali kuhusu matukio yatakayofuata yatakuwaje. Hivyo, ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo humfanya mtazamaji kuwa na shauku ya kujua kinachofuata baada ya tukio la mwanzo kumalizika . Hii ni kutokana na hali ambayo mwigizaji au waigizaji jinsi wanavyotenda ufundi wao wakiwa jukwaani jambo ambalo husababisha hadhira kuwa na shauku ya kufuatilia igizo hilo. Kwa mfano, igizo la *Safari ya Gwalu* msanii anasema:

(Wakati Gwalu akiwa kwenye mashindano kati ya darasa la 5A na darasa la 5F. Mchuano baina ya madarasa hayo ulionekana kuwa mkali. Mwalimu mmoja alisimamia mashindano hayo kama ifuatavyo)
**Mwalimu:** Si mnajua leo ndio ile siku ya mashindano jamani
**Wa'nzi wote:** Ndiooo
**Mwalimu:** Kati ya darasa la 5A na darasa la 5F.
**Wanafunzi:** Ndioo!

**Mwalimu:** La 5A mtashindaa?
**Wanafunzi:** Ndioo.
**Mwalimu:** Na la 5F je mtashinda?
**Wanafunzi:** Ndio.
**Mwalimu:** Kwa hiyo tunaanza kuuliza maswali sawa jamani.

**(Igizo la Safari ya Gwalu, sehemu ya 4, dk. 12:36 - 13: 27*)***

Tukio hilo linawapa shauku watazamaji kutaka kujua matokeo ya mashindano baina ya darasa la 5A na darasa la 5F yatakuwaje? Je, ikitokea darasa la 5F likashindwa, Gwalu atafukuzwa shule au ataruhusiwa kuendelea na masomo yake kutokana na ushirikiano mzuri aliokuwa nao kati yake na wanafunzi wenzake? Ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ndio huibua dhima ya taharuki kwa watazamaji wa maigizo; ndiyo maana, katika igizo la *Bado Natafuta* msanii ameendelea kuiweka bayana dhima ya taharuki kwa watazamaji kwa kusema:

(Tukio la birthday lililofanyika nyumbani kwao Patricia lilisababisha kutokea ajali ya umeme kwa mhusika James, ambaye alitakiwa kupeleka maji safi kwa ajili ya matumizi ya familia. Kwa bahati mbaya alikanyaga waya wa umeme uliolazwa chini na kuanguka kwa mshituko mkubwa na kuzimia hapo hapo)

**Patricia:** Kwa hiyo mashine imekataa kupandisha maji huko juu.
**Mlinzi:** Eee, ndio kama unavoona maana nimejitahidi ila nimeshindwa.
**Patricia:** Sasa babu inabidi uvizie wale vijana wanouza kwa mkokoteni walete ili tujaze hata pipa mbili. Tutaaibika!
**Mlinzi:** Sawa Dokta, nitafanya hivyo.
**Patricia:** Makelele ya nini hapa?
**Mlinzi:** Maji hayo.
**Patricia:** Kwa hiyo kuleta maji ndio mpige kelele? kwani hamuoni kama kuna watu huku ndani?
**Mlinzi:** Wanabishana tu hao aanze kuingia nani, nani abaki.
**Patricia:** Leteni madumu yote ndani huku.
**Wote:** Wanaingia kupeleka maji, (mara James alipokuwa anarudi kumimina maji alijikuta akiwashangaa wageni waalikwa jinsi walivyopendeza na kusahau kuangalia chini alipokanyaga ndipo akaukanyaga waya wa umeme zilizokuwa zimewekwa chini ndio hapo ilipotokezea shoti ya umeme na kuanguka hapo hapo).
**James:** (Alipiga kelele mithili ya mtoto aliyejibana kidole chake kwenye bawaba za mlango) Aaaaa chiiiii!

**(Bado Natafuta, sehemu ya 1A, dk. 6: 7, - dk. 7: 40)**

Tukio hilo huwafanya watazamaji kutaka kufahamu hali ya James kuwa bado mzima au amefariki kutokana na shoti aliyoipata wakati wa kupeleka maji nyumbani kwa Patricia. Hivyo, ushikamani mzuri wa mandhari na jukwaa la kisasa huipa uhai kazi ya fasihi, kwani watazamaji huwa na kiu ya kutaka kujua tukio lijalo litakuwaje.

Aidha, mtoa taarifa 7 anaweka bayana dhima ya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa kwa kusema:

*Taharuki ni ile hali anayoipata mtazamaji wa maigizo ya kusisimka kwa hamu ya kutaka kujua kitakachotokea baadaye kutokana na tukio lililoisha. Hali hiyo, hufanya*

> *watazamaji wa maigizo kuvutiwa na maigizo hayo. Hii ni kutokana na mtunzi kuvisana vyema vipengele vya mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo. (**Mjadala wa Kikundi 1, Mtoa taarifa 7, 27/3/2023**)*

Maelezo hayo yanalenga kuibua taharuki kwa watazamaji wa maigizo, hii inatokana na ushikamani mzuri wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo. Hivyo, basi, kutokana na vijenzi vya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa kuwa na dhima ya kuibua taharuki, watungaji na waongozaji wa maigizo ya kisasa, hawana budi kuvishikamanisha vyema ili kuibua taharuki kwa hadhira na kusababisha kuongeza wigo wa hadhira inayofuatilia maigizo hayo.

**Kudhihirisha Maendeleo ya Maigizo ya Kiswahili**

Moja ya mambo yanayoonesha maendeleo katika maigizo ni hali ya maigizo hayo kutumia zana za sayansi na teknolojia katika uwasilishwaji wake; kupitia runinga na mitandao ya kijamii (Qassim, 2022). Nukuu hiyo inamaanisha kuwa maigizo ya Kiswahili yamepiga hatua kutoka uwasilishwaji wa jukwaa la asili ambapo hadhira na fanani kuwa pamoja.

Kwa sasa, ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa umefanya maigizo kuwa na haiba mpya, kwani uwasilishaji wake umekuwa kwa njia ya runinga au mitandao ya kijamii. Kama inavyofafanua nadharia teule ya makala hii kupitia mhimili unaoelezea dhima ya fasihi kupitia utamaduni ni muhimu katika kubainisha mila na desturi za jamii kwa mujibu wa mabadiliko ya jamii hiyo. Hivyo, ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa umeibuliwa na mabadiliko ya jamii kutokana na athari za sayansi na teknolojia. Kwa mfano maigizo teule yamewasilishwa kwa njia ya video:




**Picha na. 3 & 4, zinazoonesha sehemu za video katika maigizo teule**

Picha hizo zinaonesha kuwa fasihi ni kama kazi nyingine za kisanaa hazituami katika hali moja, bali kila siku hupata maendeleo. Maelezo hayo yanaakisi picha za hapo juu, kwani picha ya kwanza upande wa kushoto inaonesha mandhari ya skulini pamoja na jukwaa la kisasa, ambapo anaonekana Gwalu amesimama mbele ya darasa huku mwalimu ameegemea meza na wanafunzi wenzake wamekaa kwenye madawati. Hivyo, ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa umejidhihirisha kupitia igizo teule, kwani jukwaa lake limepata sura nyingine kutoka jukwaa asilia kuwa jukwaa la kisasa kutokana na kushikamana na mandhari.

Halikadhalika, katika picha ya pili upande wa kulia inaonesha maendeleo ya sayansi yaliyofikiwa katika maigizo ya Kiswahili kupitia ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika igizo teule. Picha ya hapo juu inaonesha wazi James amekaa na Patricia katika mazingira ya bustanini huku wakizungumza masuala yao ya kimapenzi. Hivyo, kuhama kwa jukwaa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ni maendeleo ya jukwaa la maigizo, kwani awali jukwaa asilia lilikuwa sehemu moja tu lakini kwa sasa jukwaa la kisasa huhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine kutokana na tukio la uigizaji kuwa halisia. Kwa maana hiyo, vijenzi vya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo teule vimeibua dhima ya maendeleo ya maigizo ya Kiswahili. Hali hiyo imesawiriwa pia na mtoa taarifa 1 pale aliposema:

> *Ushikamani wa vijenzi vya mandhari na jukwaa la kisasa ni sehemu ya makuzi na maendeleo ya maigizo ya Kiswahili, kwa vile kila siku kazi za fasihi hukua na kupanuka kitanzu na kimwonekano. Wewe huoni, hapo mwazo tulikuwa tunaangalia maigizo kwenye kumbi za maonesho tu, lakini sasa ni wewe na muda wako, kwani video zake zinapatikana kwa njia uitakayo. (**Mjadala wa Kikundi 1, Mtoa taarifa 1, 27/3/2023**)*

Maelezo hayo yanathibitisha dhima ya maendeleo ya maigizo, hii imesababishwa na ushikamani mzuri wa mandhari na jukwaa la kisasa katika uwasilishaji wa maigizo. Yaani, vijenzi vya ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa vimekuwa sababu ya dhima ya maendeleo ya maigizo katika fasihi ya Kiswahili. Kama asemavyo Mganga (2021) kuwa kwa sasa kuna aina tatu za maigizo; maigizo ya watoto, ya jukwaani na ya studioni. Maigizo ya studioni ni aina mpya ya maigizo ya Kiswahili iliyotokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na kulazimisha mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo kushikamanishwa, hatimaye kuibua dhima ya maendeleo ya maigizo hayo.

Kwa ujumla ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya Kiswahili huyafanya maigizo kuwa na mvuto kwa watazamaji kwani mshikamano wa vipengele hivyo wakati wa uwasilishaji wa tukio la uigizaji huwafanya hadhira wazidi kuipenda sanaa ya maigizo.

## Hitimisho

Matokeo yanaonesha kuwa; kujenga uhalisi, kuleta mvuto kwa hadhira, kujenga taharuki na kudhihirisha maendeleo ya maigizo ya Kiswahili ndiyo dhima zinazodhihirishwa na ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo teule. Hii ina maana kwamba kushikamana kwa vipengele vya mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya teule ya Kiswahili ya studioni kuna tija kubwa kwa hadhira na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla wake, kwani bila ya ushikamani huo maigizo ya zama hizi za sayansi na teknolojia yangekosa mvuto, uhalisia, taharuki na hata fasihi yenyewe ingekuwa imetuama kimaendeleo. Hivyo, utafiti huu unaweza kutumika kama kielelezo kwa wachambuzi, watunzi na waigizaji wa maigizo kutokana na matokeo ya utafiti yaliyopatikana katika kuchunguza ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ya Kiswahili.

Makala hii inapendekeza yafuatayo: Mosi, tafiti nyingi zifanyike kuhusiana na maigizo ili ziweze kubainisha yale yote yenye uhusiano na maigizo, hususani katika vipengele vya fani kama vile kipengele mtindo. Pili, watungaji na waigizaji wa maigizo wapewe elimu ya kutosha kuhusiana na ushikamani wa mandhari na jukwaa la kisasa katika maigizo ili kuleta mvuto wa kazi kwa watazamaji. Tatu, uchambuzi na uhakiki wa kazi za kifasihi kama vile maigizo hauna budi kutazamwa kwa jicho pana ili ziweze kukidhi matakwa ya watazamaji.

**MAREJELEO**

Bauman, Z. (1989). Modernity and the Holocaust. Oxford: Polity Press.
Foley, J. M. (1995). The singer of tales in parformance. Indian University Press.
Gituku, N. (1990). Maigizo ya kienyeji ya watoto nchini Kenya. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
Issa, S. A. (2023). Bado natafuta na safari ya Gwalu. (Mahojiano ya simu kutoka kwa mtafiti tarehe 14 / 2 / 2023. Muda: 8: 30 mchana).
Kahuro, K. K. (2018). The art of stage directing: A case of three Kenyan Directors. In The School of Creative Arts, Film & Media Studies of Kenyatta University.
Kantangayo, K. (2011). Matumizi ya lugha za sanaa ya Kiswahili katika kazi za sanaa. East African Publishers.
Madumulla, J. S. (2009). Riwaya ya Kiswahili. Nadharia, historia na misingi ya Uchambuzi. Phoenix.
Mulokozi, M. M. (2017). Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili. KAUTTU.
Mutegi, L. (2010). Maigizo katika fasihi simulizi: Mfano wa kirarire katika nyimbo za tohara za wameru. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
Mganga, N. A. (2021). Kifani cha fasihi neni. Karljamer Publishers Limited
Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa fasihi nadharia na mbinu. Jomo Kenyatta Foundation Ltd.
Ponera, A. S. (2019). Misingi ya utafiti wa kitaamuli na uandishi wa tasnifu. Central Tanganyika Press.
Qassim, A. R. (2022). Mustakabali wa malezi ya watoto katika vichekesho teule vya Mai Zumo na Dogo Sele. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Waislam cha Morogoro: Tanzania.
Samweli, M. (2015). Umahiri wa Kiswahili. MEVELI Publishers.
Simbi, I, Wasike, M. & Amukowa, D. (2019). Matumizi ya maigizo kama mbinu ya kufundisha tamthilia katika shule za upili, kaunti ya Bungoma Kusini, Kenya: Kibabii University.
Wamitila, K. W. (2003). Kichocheo cha fasihi: simulizi na andishi. Kenya Focus Publication Ltd.
Wanjala, F. S na Kavoi (2011). Mbinu za mawasiliano na ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Serengeti Bookshop.
Wafula, R. M. &Njogu, K. (2007). Nadharia za uhakiki wa fasihi. Jomo Kenyatta Foundation.
Wamitila, K. W. (2002). Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake. Nairobi Phoenix Publishers Limited.